

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA**

**10 MEI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 10 MEI, 2021


I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya  
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee  
na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:



**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**215. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE  
(LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvutia  
Wawekezaji katika kilimo cha Parachichi  
Mkoani Njombe.

## **OFISI YA RAIS TAMISEMI:**

### **216. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara katika Mji wa Mbinga.

### **217. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIAS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kairuki hadi *Mikocheni Shoppers* ambayo hadi sasa imejengwa kipande kidogo.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

### **218. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha kuwa kunajengwa Kiwanda cha kuchakata Viungo Wilayani Muheza.

**WIZARA YA MADINI:**

**219. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni kwanini Mgodu wa Mwadui *Williamson Diamond Ltd* umesimamisha shughuli za uzalishaji wa Almasi kwa muda mrefu na ni lini Mgodu huo utaanza uzalishaji tena.

**WIZARA YA KILIMO:**

**220. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

- (a) Je, ni nini kinasababisha Tanzania kutojitosheleza kwa Mafuta ya Kula;
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mikoa yenye Ardhi ya kutosha ya kuzalisha Zao la Alizeti hususan Mkoa wa Mara inatambuliwa rasmi na kupewa mahitaji yote ya mbegu.



## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **221. MHESHIMIWA JACQULINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Lumecha – Londo – Kilosa kwa Mpepo inayounganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro kwa kiwango cha lami.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **222. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wananchi wanaoishi kwenye Vijiji vinavyopakana na Hifadhi pamoja na mali zao wanakuwa salama kwani Wanyamapori wamekuwa wakiingia na kufanya uharibifu kwenye Vijiji.

**223. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni upi Mpaka sahihi wa Bonde la Kilombero kati ya Mpaka uliowekwa Mwaka 2012 na ule uliowekwa Mwaka 2017.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
10 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**